

20.06.2018

TANGAZO

NUKUU YA BEI KWA AJILI YA MAFUNDI WATAKAOJENGA MAJENGO YA SHULE YA SEKONDARI VUDOI

1. Halmashauri ya wilaya ya Mwangi imepokea fedha za ujenzi majengo ya shule ya sekondari Vudoi, hivyo basi anawatangazia mafundi walioko ndani ya wilaya kutoa huduma ya ujenzi wa madarasa manne (4) na mabweni mawili (2) katika shule ya sekondari Vudoi.
2. Tangazo hili la kupata mafundi liko wazi kwa mafundi wote waliopo ndani ya wilaya ya Mwangi .
3. Mwombaji awe na vifaa vote vya kazi ya ujenzi vya kutosha.
4. Mwombaji atatakiwa kuorodhesha kazi alizokwishafanya na anazoendelea kufanya kwa kipindi cha mwaka 1 uliopita na thamani ya kazi hizo.
5. Tathmini itazingatia masharti yaliyoainishwa kwenye tangazo husika.
6. Mwisho wa kutuma maombi ni Jumatatu tarehe 25/06/2018 saa 4.30 asubuhi.maombi yote yakiwa yamefungwa kwenye bahasha yenye lakiri na isiyo na alama ya kutambulisha aliyeomba.
7. Maombi yanatakiwa yawe yameshatumwa kwa kuletwa kwa mkono kwenye ofisi ya Mkuu wa shule Vudoi sekondari au kuwasilisha kwa kutuma kupitia anuani ya Shule , **Mkuu wa shule Vudoi sekondari S. L.P 157 MWANGA.**
8. Mafundi watakaotaka kuomba kazi hii ya ujenzi wafike ofisi ya Mkuu wa shule Vudoi sekondari, kwa ajili ya maelekezo zaidi na kuchukua ramani ya majengo na kuona eneola ujenzi .
9. Nukuu za bei zitakazoletwa baada ya muda kuisha hazitapokelewa wala kufunguliwa .
10. Watumishi wa Halmashauri na waheshimiwa madiwani Hawaruhusiwi kuomba kazi hii.
11. Mwombaji harusiwi kuomba kazi zaidi ya moja.
12. Mwombaji ajaze gharama zake kwa kujaza jedwali lililo ambatanishwa hapo chini.


MKUU WA SHULE

VUDOI SEKONDARI

MWANGA.

